**HOTBA YA IJUMAA**

**الأشهر الحرم رسالة سلام للإنسانية**

**Miezi mitukufu ni ujumbe wa amani kwa wanadamu**

**Imefasiriwa**

**Na**

**Profesa Ayman Alasar**

Shukrani njema zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, msemaji ndani ya Kitabu chake:

**إِنَّ عِدَّةَ الشُّهُورِ عِنْدَ اللَّهِ اثْنَا عَشَرَ شَهْرًا فِي كِتَابِ اللَّهِ يَوْمَ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ مِنْهَا أَرْبَعَةٌ حُرُمٌ ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ.**

{**Hakika idadi ya miezi kwa Mwenyezi Mungu ni miezi kumi na mbili katika hukumu ya Mwenyezi Mungu tangu alipo umba mbingu na ardhi. Katika hiyo iko mine mitakatifu. Hiyo ndiyo Dini iliyo sawa**}.

Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika. Na ninashuhudia kuwa Mtume Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma amani na baraka kwake Mtume pamoja na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale waliowafuata kwa wema mpaka siku ya kiyama.

**Baada ya Utangulizi**:

miongoni mwa fadhila za Mwenyezi Mungu kwa waja wake ni pamoja na kuwateulia misimu bora na yenye baraka, ndani ya misimu hiyo malipo huwa mara dufu na waja kufutiwa madhambi, ambapo Anasema Mola wa haki utakasifu ni wake**: وَذَكِّرْهُمْ بِأَيَّامِ اللَّهِ** {**Na wakumbushe siku za Mwenyezi Mungu**}.

Na anasema Mtume S.A.W: "*Hakika kwa Mola wenu Mtukufu ndani ya masiku yenu ya mwaka kuna utoaji wa Mwenyezi Mungu, hivyo jiwekeni kwenye utoaji*

*huo kwani huenda mmoja wenu akapata kwenye utoaji huo na akawa baada ya hapo si muovu tena*"

Miongoni mwa misimu hii ya kiimani ya miezi mitukufu ameiashiria Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ujumla ndani ya kauli yake:

**إِنَّ عِدَّةَ الشُّهُورِ عِنْدَ اللَّهِ اثْنَا عَشَرَ شَهْرًا فِي كِتَابِ اللَّهِ يَوْمَ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ مِنْهَا أَرْبَعَةٌ حُرُمٌ ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ فَلَا تَظْلِمُوا فِيهِنَّ أَنْفُسَكُمْ.**

{**Hakika idadi ya miezi kwa Mwenyezi Mungu ni miezi kumi na mbili katika hukumu ya Mwenyezi Mungu tangu alipo umba mbingu na ardhi. Katika hiyo iko mine mitakatifu. Hiyo ndiyo Dini iliyo sawa hivyo msizidhulumu nafsi zenu ndani ya miezi hiyo**}. Mtume wetu akabainisha kwa ufafanuzi zaidi kwenye hija ya kuaga pale aliposema: "*Fahamuni kuwa muda umebadilika kama ulivyokuwa Mwenyezi Mungu alipoumba mbingu na ardhi, mwaka una miezi kumi na miwili, katika miezi hiyo kuna miezi minne mitukufu, mitatu ni yenye kufuatana ambayo ni: Mfungo pili, mfungo tatu na mfungo nne, na mfungo kumi unapatikana kati ya mfungo tisa na shabani*".

Miezi mitukufu ni yenye utukufu na sehemu takatifu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, imeitwa miezi mitukufu ni kutokana na ukubwa wa utukufu wake, hivyo Sharia imekuja kwa kuharamisha vita ndani ya miezi hiyo na kukiuka yaliyokatazwa ni katika haramu kubwa, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

**يَسْأَلُونَكَ عَنِ الشَّهْرِ الحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ قُلْ قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ.**

{**Wanakuuliza kuhusu kupigana vita katika mwezi mtakatifu. Sema: Kupigana vita wakati huo ni dhambi kubwa**}. Hivyo miezi mitukufu inabeba ujumbe wa amani kwa wanadamu wote kuwa dini ya Kiislamu ni dini ya amani, na amani ni jina katika majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambapo Mola Mtukufu Anasema: **هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْمَلِكُ الْقُدُّوسُ السَّلَامُ** {**Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye tu. Mfalme, Mtakatifu, Mwenye Amani**}. Na Mtume wetu Muhammad S.A.W ni Mtume wa huruma na amani

ambapo Mwenyezi Mungu Anasema: وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ {**Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehma kwa walimwengu wote**} na ilikuwa miongoni mwa maombi ya Mtume S.A.W baada ya kila swala akisema:

**اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلاَمُ وَمِنْكَ السَّلاَمُ تَبارَكْتَ يا ذَا الْجَلاَلِ وَالإِكْرَامِ.**

"*Ewe Mwenyezi Mungu wewe ndio mwenye amani na kwako ndiko kwenye amani umetukuka ewe mwenye utukufu na ukarimu*".

Hivyo Uislamu si wenye kupenda vita wala umwagaji damu bali wenyewe unazuia mambo hayo kila inapopatikana njia na sababu ya hilo, na hufungua mkono wake wa amani na kusisitiza amani, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

**وَإِنْ جَنَحُوا لِلسَّلْمِ فَاجْنَحْ لَهَا وَتوَكَّلْ عَلَى اللهِ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ العَلِيمُ.**

{**Na wakielekea kwenye amani nawe pia elekea, na mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua**}. Na Mtume S.A.W anasema: **لاَ تَتَمَنَّوْا لِقَاءَ الْعَدُوِّ، وَسَلُوا اللهَ الْعَافِيَةَ، فَإِذَا لَقِيتُمُوهُمْ فَاصْبِرُوا** "*Msitamani kukutana na adui, na muombeni Mwenyezi Mungu afya, ikiwa mtakutana nao basi subirini*", ujumbe wa Uislamu na ujumbe wa amani ni pacha wawili na lengo lake ni kuleta furaha kwa watu wote, kwani Mola Mtukufu Anasema:

**يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَى وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ اللَّهِ أتقاكم إن الله عليم خبير.**

{**Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamme na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliyemcha-Mungu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua zaidi, Mwenye habari**}.

***

**HOTUBA YA PILI**

Namshukuru Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote, sala na salamu zimwendee mbora wa viumbe Mtume wetu Muhammad pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Kutukuza miezi mitukufu kunahitaji kujizuia na aina zote za ugaidi siasa kali na kumwaga damu za watu wa amani na kuwatisha, kama vile kunahitaji kujikubalisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa uwingi wa matendo ya utiifu, hivyo ni jukumu letu kuitukuza miezi hii na masiku haya kwa kufanya jitihada katika ibada na kutakasa nafsi kwa kufanya matendo ya utiifu na ya kujiweka karibu, ambapo Mola Mtukufu Anasema: **وَافْعَلُوا الخَيْرَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ** {**Na fanyeni mambao ya heri ili mpate kufaulu**} na Mtume S.A.W anasema:

**صُمْ مِنَ الحُرُمِ وَاتْرُكْ، صُمْ مِنَ الحرُم وَاترُكْ، صُمْ مِنَ الحرُمِ وَاتْرُكْ.**

“Funga ndani ya miezi mitukufu na uache, Funga ndani ya miezi mitukufu na uache, Funga ndani ya miezi mitukufu na uache”.

Miongoni mwa miezi hii mitukufu ni mwezi wa mfungo kumi, nao umeitwa kwa jina la Rajab ni kutokana na kutukuzwa, kwani Waarabu walikuwa wanauita kwa jina la mkimya hii kwa sababu hajawahi kusikia sauti ya vita ndani ya mwezi huu, nao ni mwezi umebeba muujiza wa kupelekwa Mtume S.A.W safari ya usiku, kwa maana ya safari ya usiku ya kupelekwa Palestina na kisha kupandishwa mbinguni, nao ni ufunguo wa miezi yenye heri na baraka, kwani Abubakri Al-Warraq R.A anasema: “Mwezi wa mfungo kumi ni mwezi wa kulima, na mwezi wa shaabani ni mwezi wa kumwagilia, mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa mavuno”.

Ni uzuri ulioje kutumia vizuri miezi mitukufu katika kumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuijenga ardhi, na kufanya kazi kwa weledi pamoja na kufanya matendo mengi ya heri, kulisha chakula na kueneza roho ya huruma, ambapo Mtume S.A.W anasema:

**أَحَبُّ النَّاسِ إلى اللهِ أنفعُهم للناسِ، وأَحَبُّ الأعمالِ إلى اللهِ (عزَّ وجلَّ) سرورٌ تُدخِلُه على مسلمٍ، تَكشِفُ عنه كُربةً، أو تقضِي عنه دَيْنًا، أو تَطرُدُ عنه جوعًا، ولأَنْ أمشيَ مع أخٍ في حاجةٍ؛ أَحَبُّ إليَّ**

مِنْ أَنْ أَعْتَكِفَ فِي هَذَا المَسْجِدِ – يَعْنِي: مَسْجِدَ المَدِينَةِ – شَهْرًا، وَمَنْ كَظَمَ غَيْظَهُ وَلَوْ شَاءَ أَنْ يُمْضِيَه أَمْضَاهُ؛ مَلَأَ اللهُ قَلْبَهُ يَوْمَ القِيَامَةِ رِضًا، وَمَن مَشَى مَعَ أَخِيهِ فِي حَاجَةٍ حَتَّى يَقضِيَها لَهُ؛ ثَبَّتَ اللهُ قَدمَيْهِ يَوْمَ تَزُولُ الأَقْدَامُ.

“*Mtu mwenye kupendwa zaidi na Mwenyezi Mungu ni yule mwenye kuwafaa zaidi watu, na matendo mazuri yanayopendwa na Mwenyezi Mungu Mtuukufu ni furaha inayoingizwa kwenye moyo wa Muislamu, anaondolewa shida au kulipiwa deni au kuondoshewa njaa, na mtu kushuhurikia mahitaji ya ndugu yake kwangu inapendeza zaidi kuliko kukaa itikafu ndani ya Msikiti huu – kwa maana ya Msikiti wa Madina – kwa muda wa mwezi mmoja, na mwenye kuzuia hasira zake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu pamoja na kuwa na uwezo wa kutozizuia basi Mwenyezi Mungu ataujaza moyo wake ridha siku ya Kiyama, na mwenye kushuhurikia mahitaji ya ndugu yake mpaka akamsaidia basi Mwenyezi Mungu atathibitisha miguu yake siku miguu itakapo dondoka*”.

**Ewe Mwenyezi Mungu tubariki ndani ya mwezi wa mfungo kumi na mwezi wa Shaabani na utufikishe mwezi wa Ramadhani.**